



TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA

JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI

MTAALA WA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI

FASIHI YA KISWAHILI

GREDI YA 11

OKTOBA, 2025

Toleo la Kwanza 2025

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

ISBN: 978-9914-43-085-1

Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

YALIYOMO

MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA.....	ii
DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI KATIKA MTAALA WA KIUMILISI.....	iv
MATOKEO YA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI.....	iv
ORODHA YA MASOMO KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI.....	v
MGAO WA VIPINDI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI.....	vi
KAULI KIINI.....	vii
MATOKEO YA JUMLA YA SOMO LA FASIHI YA KISWAHILI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI.....	viii
MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO.....	ix
MADA NA MADA NDOGO.....	1
VIGEZO NA VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHMINI.....	63
MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI.....	67

MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

- Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kutatua mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.
- Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.
 - Mahitaji ya kijamii**
Elimu nchini Kenya lazima iwatayarisha vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya usasa yanayojitokeza kwa kasi. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kuwa na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko haya.
 - Mahitaji ya kiuchumi**
Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na uwezo wa kibinafsi unaohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.
 - Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya kasi ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunahitaji kuwa sehemu ya maendeleo haya ili mfumo wetu wa elimu ulenge kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko yanayoendelea ulimwenguni.
- Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.
5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa. Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.
6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Watoto wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.
7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
Kenya ni sehemu ya jamii ya kimataifa. Ni sehemu ya mtandao changamano unaotegemeana wa watu na mataifa. Kwa hivyo, elimu inapaswa kuwaelekeza vijana kukubali uanachama wa jamii hii ya kimataifa pamoja na majukumu na uwajibikaji, haki na manufaa ambayo yanatokana na uanachama huu.
8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

iii

DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI KATIKA MTAALA WA KIUMILISI

Daraja ya Juu ya Shule za Upili, ni kiwango cha nne cha Elimu ya Msingi katika Mtaala wa Kiumilisi (CBC) ambayo wanafunzi watajiunga nayo baada ya kumaliza Chekechea, Shule ya Msingi, na Shule ya Junia. Lengo kuu la Daraja ya Shule za Upili ni kuwapa wanafunzi uzoefu wa awali wa chuo kikuu au taaluma, ambapo wanafunzi wanapata fursa ya kuchagua mielekeo na nyanja wanazovutiwa nazo na walizoonyesha uwezo katika viwango vya awali. Daraja ya Juu ya Shule za Upili inajumuisha miaka mitatu ya masomo kwa wanafunzi walio kati ya umri wa miaka 16-18 na huweka msingi wa elimu ya juu zaidi, mafunzo ya kitaaluma, na ulimwengu wa kazi. Katika ruwaza ya Mtaala wa Kiumilisi, wanafunzi watakaohitimu katika kiwango hiki wanatarajiwa kuwa raia waliohusishwa, waliowezeshwa, na waadilifu walio tayari kushiriki katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya taifa.

Katika kiwango hiki, wanafunzi watajifunza masomo saba (7) kama yalivyopendekezwa na Kamati ya Rais ya Mageuzi ya Elimu (PWPER, 2023). Masomo haya yanajumuisha masomo manne ya lazima ambayo ni: English, Kiswahili, Essential Mathematics/Core Mathematics na Community Service Learning – CSL. Wanafunzi watachagua kati ya Core Mathematics (kwa wanafunzi wanaofuatilia mkondo wa STEM) na Essential Mathematics (kwa wanafunzi wanaofuatilia mikondo isiyo ya STEM). Wanafunzi watachagua masomo mengine matatu kulingana na chaguo la taaluma, vipaji, mapendeleo yao kwa somo fulani, na haiba zao, wakisaidiwa na mwalimu wao wa Daraja ya juu shule za upili.

MATOKEO YA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

Kufikia mwisho wa Daraja ya Juu ya Shule za Upili, mwanafunzi aweze:

1. Kuwasiliana ipasavyo na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika miktadha mbalimbali.
2. Kutumia maarifa ya kihisabati, kimantiki na uwazaji kina katika utatuzi wa matatizo.
3. Kutumia maarifa ya kimsingi ya utafiti na sayansi kudhibiti mazingira yake na kutatua matatizo.
4. Kutumia vizuri vipaji mbalimbali kwa ajili ya burudani, kujiendeleza kitaaluma, kielimu pamoja na kimafunzo.
5. Kudumisha tunu za kitaifa, kimaadili na kidini katika maisha ya kila siku.
6. Kutumia na kuendeleza mikatiji ya matunzo ya kiafya katika maisha ya kila siku.
7. Kulinda, kuhifadhi na kuboresha mazingira kwa ajili ya uendeleu.
8. Kudhihirisha uraia wa kitaifa na wa kimataifa kwa ajili ya utangamano wa kindugu.
9. Kuonyesha uthamini wa tofauti za watu na tamaduni.
10. Kuonyesha uwajibikaji katika kushughulikia masuala mtambuko.

iv

ORODHA YA MASOMO KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

Core Subjects	Arts & Sports Science	Social Sciences	Science, Technology, Engineering & Mathematics (STEM)
1. English 2. Kiswahili/KSL 3. Core Mathematics/ Essential Mathematics 4. Community Service Learning (CSL)	5. Sports and Recreation 6. Music and Dance 7. Theatre and Film 8. Fine Arts	9. Literature in English 10. Indigenous Languages 11. Fasihi ya Kiswahili 12. Sign Language 13. Arabic 14. French 15. German 16. Mandarin Chinese 17. Christian Religious Education 18. Islamic Religious Education 19. Hindu Religious Education 20. Business Studies 21. History and Citizenship 22. Geography	23. Biology 24. Chemistry 25. Physics 26. General Science 27. Agriculture 28. Computer Studies 29. Home Science 30. Aviation 31. Building Construction 32. Electricity 33. Metalwork 34. Power Mechanics 35. Wood Technology 36. Media Technology 37. Marine and Fisheries Technology

Tanbihi

- Physical Education (PE) na Ujuzi wa Teknolojia na Mawasiliano (ICT skills) utatolewa kwa wanafunzi wote ili kuwezesha ujifunzaji na kufurahia.
- Kila shule itatoa Mpangilio wa Mafundisho ya Kidini (PPI) kwa ajili ya maendeleo ya kimaadili, kiimani na tabia njema za wanafunzi.
- Kutakuwa na somo moja kwa ajili ya usomaji wa kibinafsi au kwa makundi ili kudumisha maarifa na kuimarisha ujuzi katika maeneo yanayochaguliwa na wanafunzi.

Jedwali la 2, hapa chini linatoa mwongozo wa mgao wa vipindi katika Daraja ya Juu Shule za Upili.

v

MGAO WA VIPINDI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

SOMO	Vipindi Kwa Wiki (Dakika 40 kwa kipindi)
MASOMO YA LAZIMA 4	
1. English	5
2. Kiswahili	5
3. Physical Education (PE)	5
4. Community Service Learning (CSL)	3
Masomo ya Kuchagua/Hiari	
5. Chaguo la 1	5
6. Chaguo la 2	5
7. Chaguo la 3	5
* Physical Education	3
* ICT Skills	2
* PPI	1
* Learner Personal /Group Study	1
Jumla ya idadi ya vipindi	40

vi

KAULI KIINI

Somo la Fasihi ya Kiswahili katika Daraja ya Juu ya Shule za Upili linaendeleza maarifa na ujuzi ambao mwanafunzi amepata katika Shule ya Junia. Lengo kuu ni kumwezesha mwanafunzi kupanua uelewa wake kuhusu fasihi, si tu kama sanaa ya lugha bali pia kama chombo cha kuelewa na kushirikiana na tamaduni mbalimbali. Mabadiliko haya kutoka Shule ya Junia hadi daraja ya juu huambatana na upanuzi wa dhana, stadi, na mwelekeo wa kifasihi. Wanafunzi hujifunza kwa kina kuhusu tanzu mbalimbali za fasihi kama vile ushairi, riwaya, tamthilia, hadithi fupi, kazi za kihalisia na fasihi simulizi. Somo hili hulenga kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kwa kina, kutathmini na kuhakiki kazi za fasihi kwa kuzingatia muktadha wa kijamii, kiutamaduni na kihistoria. Aidha, somo hili huwasaidia wanafunzi kutambua nafasi ya fasihi kama sanaa ya lugha na kama chombo cha kuwasilisha, kuhifadhi, na kuendeleza maadili na tamaduni za jamii mbalimbali.

Mbinu za ujifunzaji katika somo hili zinalenga kumwandaa mwanafunzi kwa hatua inayofuata ya kielimu na kimaisha. Ufundishaji huhusisha ushirikishwaji wa wanafunzi kupitia mijadala ya kina, uchambuzi wa matini, uandishi wa kazi za kiubunifu na utekelezaji wa miradi ya kifasihi. Vilevile, wanafunzi watashiriki matukio ya kifasihi kama vile maonyesho ya kazi za kibunilizi, mashindano ya ushairi na makongamano ya kielimu ili kukuza stadi za uwasilishaji na kuwapa wanafunzi uwezo wa kufikiri kwa kina, kuwasiliana kwa ufasaha, na kushirikiana na wengine katika mazingira tofauti ya kijamii na kitaaluma. Hali hii huwajengea misingi imara ya kujiamini na kuwa raia wenye mchango chanya katika jamii yao na ulimwenguni kwa jumla.

Kufikia mwisho wa kozi, mwanafunzi anatarajiwa kuwa amefikia kiwango cha juu cha umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Hali hii itamfungulia fursa za ajira katika taaluma kama vile uandishi wa habari, tafsiri, uchapishaji, utafiti wa kifasihi, ufundishaji, sanaa za maonyesho, burudani na utangazaji.

vii

MATOKEO YA JUMLA YA SOMO LA FASIHI YA KISWAHILI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

Kufikia mwisho wa Daraja ya Juu ya Shule za Upili, mwanafunzi aweze:

1. kuwasiliana ipasavyo na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika miktadha mbalimbali
2. kutumia maarifa ya kihisabati, kimantiki na uwazaji kina katika utatuzi wa matatizo
3. kutumia maarifa ya kimsingi ya utafiti na sayansi kuboresha mazingira yake na kutatua matatizo mbalimbali
4. kutumia vizuri vipaji mbalimbali kwa ajili ya burudani, kujiendeleza kitaaluma, kielimu pamoja na kimafunzo
5. kudumisha tunu za kitaifa, kimaadili na kidini katika maisha ya kila siku
6. kutumia na kuendeleza mikakati ya matunzo ya kiafya katika maisha ya kila siku
7. kulinda, kuhifadhi na kuboresha mazingira kwa ajili ya uendelevu
8. kudhihirisha uraia wa kitaifa na wa kimataifa kwa ajili ya utangamano wa kidugu
9. kuonyesha uthamini wa tofauti za watu na tamaduni
10. kuonyesha uwajibikaji katika kushughulikia masuala mtambuko.

viii

MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO

Mada	Mada Ndogo
Fasihi Simulizi	1.1.1 Misingi ya fasihi simulizi
	2.1.1 Uchanganuzi wa hadithi: visasili na ngano za usuli
	3.1.1 Uchanganuzi wa semi: tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili
	4.1.1 Ushairi simulizi: nyimbo
	5.1.1 Uchanganuzi wa mazungumzo: mawaidha, hotuba na maapizo
	6.1.1 Uchanganuzi wa maigizo: michezo ya jukwani na michezo ya watoto
	7.1.1 Uchanganuzi wa hadithi: tarihi na kumbukumbu
	8.1.1 Uchanganuzi wa semi: lakabu na misimu
	9.1.1 Uchanganuzi wa ushairi simulizi: maghani simulizi
	10.1.1 Utafiti katika fasihi simulizi
Ushairi	1.2.1 Uainishaji wa mashairi: mishororo na vipande
	2.2.1 Uainishaji wa mashairi ya arudhi: <i>maneno, Sauti, mizani na ruwaza ya mawazo</i>
	3.2.1 Uchambuzi wa mashairi ya arudhi: maudhui na dhamira
	4.2.1 Uchambuzi wa mashairi: Maudhui na dhamira
	5.2.1 Uchambuzi wa mashairi: mandhari na wahusika
	6.2.1 Uchambuzi wa mashairi: muundo
	7.2.1 Uchambuzi wa mashairi: mtindo
	8.2.1 Uchambuzi wa mashairi: mtindo

ix

Mada	Mada Ndogo
Bunilizi na kazi za kihalisia	9.2.1 Uchambuzi wa mashairi: mistari, toni na mazaji
	10.2.1 Utunzi wa mashairi ya arudhi
	1.3.1 Utangulizi wa fasihi simulizi
	2.3.1 Uchambuzi wa tamthilia: maudhui dhamira na wahusika
	3.3.1 Uchambuzi wa tamthilia: mandhari, muundo na mtindo
	4.3.1 Uchambuzi wa riwaya: maudhui, dhamira na wahusika
	5.3.1 Uchambuzi wa riwaya: mandhari, muundo na mtindo
	6.3.1 Uchambuzi wa wasifu: maudhui na dhamira
	7.3.1 Uchambuzi wa wasifu: wasifu
	8.3.1 Uchambuzi wa hadithi fupi: maudhui, dhamira na wahusika
	9.3.1 Uchambuzi wa hadithi fupi: mandhari, muundo na mtindo
	10.3.1 Utunzi wa fasihi bunilizi na kazi za kihalisia

x

MADA NA MADA NDOGO

1.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
1.1 Fasihi Simulizi	1.1.1 Misingi ya Fasihi Simulizi <i>Fasihi Simulizi katika Jamii ya Sasa</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kujadili mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii ya sasa, b) kueleza sababu za mabadiliko katika fasihi simulizi, c) kuchangamkia fasihi simulizi katika jamii.	Mwanafunzi aelekezwe: • kumsilikiza mwalimu au mgeni mwalikwa akizungumzia mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii ya sasa, • kujadili na wenzake kuhusu mabadiliko katika fasihi simulizi, • kulinganisha fasihi simulizi ilivyowasilishwa na kuhifadhiwa katika jamii ya awali na jamii ya sasa, • kutafiti mtandaoni sababu za mabadiliko katika fasihi simulizi, • kutathmini sababu za mabadiliko katika fasihi simulizi, • kufanya wasilisho kuhusu mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii ya sasa.	1. Ni mambo gani ya fasihi simulizi yanayoibuka katika jamii ya sasa? 2. Kwa nini mabadiliko hutokea katika fasihi simulizi?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhiriki majadiliano na wenzake kujadili mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii ya sasa.				

1

• Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kutafiti kuhusu sababu za mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapojadili mabadiliko na sababu za mabadiliko katika fasihi simulizi. • Kujiamini: Mwanafunzi anapojadili ipasavyo kuhusu mabadiliko na sababu za mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii.
Maadili: • Heshima: Mwanafunzi anapowasilikiza wenzake na kuthamini sababu wanazotoa kuhusu mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii ya sasa. • Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu katika kujadili mabadiliko na sababu za mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu sababu za mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mabadiliko na sababu za mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii.
Masuala Mtambuko: • Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandao salama kuhusu sababu za mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii. • Ufundishaji rika: Mwanafunzi anapojadili na wenzake mabadiliko katika fasihi simulizi. • Uwazaji wa kiuchanganuzi: Mwanafunzi anapotathmini sababu za mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii. • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapotangamana na mgeni mwalikwa anapozungumzia mabadiliko ya fasihi simulizi katika jamii.

2

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
1.2 Ushairi	1.2.1 Uainishaji wa Mashairi ya Arudhi - Mishororo - Vipande	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kutambua aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia mishororo na vipande, - kuainisha mashairi ya arudhi kwa kuzingatia mishororo na vipande katika matini, - kuchambua aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia mishororo na vipande katika mashairi ya diwani teule, - kufurahia aina mbalimbali za mashairi ya arudhi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti mtandaoni au katika matini andishi aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia mishororo na vipande, - kutambua aina za mashairi ya arudhi katika matini kwa kuzingatia mishororo na vipande, - kuainisha mashairi ya arudhi katika matini kwa kuzingatia mishororo na vipande, - kusoma mashairi yenye aina mbalimbali za mishororo na vipande katika diwani teule, - kuigiza mashairi yenye aina mbalimbali za mishororo na vipande, - kuchambua aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia mishororo na vipande katika mashairi ya diwani teule,	- Ni mambo gani yanayozingatwa katika kueleza aina za mashairi ya arudhi? - Ni aina gani za mashairi ya arudhi unazozijua kwa kuzingatia mishororo na vipande?

			kuwasilisha uchambuzi wake wa aina mbalimbali za mashairi kwa wenzake ili wamtolee maoni yao.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake uchambuzi wake wa aina mbalimbali za mashairi. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kutafiti kuhusu aina za mashairi kwa kuzingatia mishororo na vipande. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotambua aina za mashairi kwa kuzingatia mishororo na vipande. - Kujiamini: Mwanafunzi anapochambua mashairi ipasavyo kwa kuzingatia mishororo na vipande.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapowasiliza wenzake na kuthamini michango yao katika kujadili aina za mashairi kwa kuzingatia mishororo na vipande. - Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana vizuri na wenzake kuchambua aina za mashairi katika diwani teule. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu aina za mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuwasilisha uchambuzi wake wa mashairi.				
Masuala Mtambuko: Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapotafiti aina za mashairi ya arudhi katika mtandao salama.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
1.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	1.3.1 Utangulizi wa Bunilizi na Kazi za Kihalisia	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza nafasi ya bunilizi na ya kazi za kihalisia katika jamii, b) kuchanganua nafasi ya bunilizi na ya kazi za kihalisia katika jamii, c) kufurahia usomaji wa bunilizi na kazi za kihalisia katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi aelekezwe: • kutafiti katika matini andishi au kusakura mtandaoni ili kubainisha nafasi ya bunilizi katika jamii, • kujadili nafasi ya bunilizi katika jamii, • kutathmini nafasi ya kazi mbalimbali za bunilizi alizosoma hapo awali, (<i>k.v. tamthilia, riwaya na hadithi fupi</i>) • kulinganisha matukio katika bunilizi aliyosoma na matukio katika maisha ya kila siku katika jamii, • kutafiti katika matini andishi au kusakura mtandaoni ili kubainisha nafasi ya kazi za kihalisia katika jamii, • kujadili nafasi ya kazi za kihalisia katika jamii akiwa na wenzake, • kutathmini nafasi ya kazi za kihalisia kwa kurejelea kazi alizosoma hapo awali (<i>k.v. Tawasifu</i>),	1. Kazi za bunilizi ulizosoma zimekufaa vipi kuielewa jamii yako? 2. Kwa nini tunasoma kazi za kihalisia?

			• kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatolee maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:				
• Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapowasilisha matokeo ya utafiti wake kuhusu nafasi ya bunilizi katika jamii kwa wenzake ili wayatolee maoni. • Kujiamini: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake matokeo ya utafiti wake ili wayatolee maoni. • Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti maktabani na mtandaoni ili kubainisha nafasi ya bunilizi katika jamii. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kubainisha nafasi ya bunilizi katika jamii.				
Maadili:				
• Heshima: Mwanafunzi anapotoa maoni kwa heshima kuhusu nafasi ya fasihi bunilizi katika jamii. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposakura kwenye mtandao salama ili kubainisha nafasi ya bunilizi katika jamii. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili nafasi ya bunilizi katika jamii.				
Masuala Mtambuko:				
• Ufundishaji rika: Mwanafunzi anapojadili na wenzake nafasi ya kazi za kihalisia katika jamii. • Uwazaji wa kiuchanganuzi: Mwanafunzi anapotathmini nafasi ya kazi mbalimbali za bunilizi alizosoma hapo awali.				

2.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
2.1 Fasihi Simulizi	2.1.1 Uchanganuzi wa Hadithi - Visasili - Ngano za Usuli	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya visasili na ngano za usuli katika fasihi simulizi ili kuzibainisha, - kufafanua sifa za visasili na ngano za usuli katika fasihi simulizi, - kujadili dhima ya visasili na ngano za usuli katika jamii, - kujadili vipengele vya visasili na ngano za usuli, - kuchanganua matini za visasili na ngano za usuli kwa kuzingatia vipengele vyake,	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya visasili na ngano za usuli katika fasihi simulizi, - kusikiliza masimulizi ya visasili na ngano za usuli kwenye kifaa cha kidijitali, - kufafanua sifa za visasili na ngano za usuli kutokana na matini alizosikiliza ili kuzipambanua, - kutafiti mtandaoni au maktabani kuhusu dhima za visasili na ngano za usuli katika jamii, - kujadili na wenzake dhima ya visasili na ngano za usuli katika jamii, - kujadili na wenzake vipengele vya visasili na ngano za usuli, - kuchanganua matini za visasili na ngano za usuli kwa kuzingatia vipengele vyake,	- Je, ni mambo gani yanayotofautisha visasili na ngano za usuli? - Visasili na ngano za usuli zina mchango gani katika jamii?

		f) kufurahia visasili na ngano za usuli katika jamii.	kusimulia visasili na ngano za usuli akiwa na wenzake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili dhima ya visasili na ngano za usuli. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapofafanua sifa za visasili na ngano za usuli. - Ubunifu: Mwanafunzi anaposimulia visasili na ngano za usuli akiwa na wenzake. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu umuhimu wa visasili na ngano za usuli katika jamii.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa visasili na ngano za usuli katika jamii. - Heshima: Mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu dhima ya visasili na ngano za usuli katika jamii.				
Masuala Mtambuko: - Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu umuhimu wa visasili na ngano za usuli katika jamii. - Uraia: Mwanafunzi anaposimulia visasili na ngano za usuli kutoka jamii yake. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposimulia visasili na ngano za usuli kutoka katika jamii yake.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
2.2 Ushairi	2.2.1 Uanishaji wa Mashairi ya Arudhi - Maneno - Sauti - Mizani - Ruwaza ya Mawazo	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo, - kuainisha mashairi arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo katika matini, - kuchambua aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo katika diwani teule, - kuchangamkia aina za mashairi arudhi katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo, - kutazama video inayoonyesha namna mbalimbali ya kuainisha mashairi ya arudhi, - kusoma matini ya mashairi arudhi na kuyaaishia kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo, - kujadili aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo akiwa na wenzake, - kuchambua aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo katika diwani teule.	Ni mambo gani unayozingatia katika kuainisha mashairi ya arudhi?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu aina za mashairi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo.				

- Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifa cha kidijitali kutazama video inayoonyesha namna mbalimbali za kuainisha mashairi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposoma matini ya mashairi ili kuyaaishia. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua mashairi ya arudhi katika diwani teule.
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapowasiliza wenzake na kuthamini michango yao katika kujadili aina za mashairi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama video kuhusu namna mbalimbali za kuainisha mashairi. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutazama video kuhusu namna mbalimbali za kuainisha mashairi.
Masuala Mtambuko: - Ufundishaji rika: Mwanafunzi anapojadili aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo akiwa na wenzake. - Mawasiliano yenye ufanisi: Mwanafunzi anapojadili aina za mashairi ya arudhi kwa kuzingatia maneno, sauti, mizani na ruwaza ya mawazo akiwa na wenzake.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
2.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	2.3.1 Uchambuzi wa Tamthilia - Maudhui - Dhamira - Wahusika	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya maudhui, dhamira na wahusika katika tamthilia, - kutambua maudhui, dhamira na wahusika katika tamthilia teule, - kuchambua maudhui, dhamira na wahusika katika tamthilia teule, - kuchangamkia uchambuzi wa maudhui, dhamira na wahusika katika tamthilia.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya maudhui, wahusika na dhamira katika fasihi, - kusoma tamthilia teule na kutambua maudhui na dhamira, - kuchambua maudhui na dhamira katika tamthilia teule, - kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu maudhui na dhamira. - kutambua wahusika katika tamthilia teule, - kujadili mambo yanayochangia uhusika katika tamthilia (<i>k.v. vitendo, mazungumzo, mawazo na malengo</i>). - kujadili sifa za wahusika katika tamthilia teule, - kuchanganua umuhimu wa wahusika katika tamthilia teule,	- Mambo yanayozungumziwa katika tamthilia yanaweza kuathiri vipi jamii? - Wahusika huendeleza vipi maudhui katika tamthilia?

			- kujadili mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika katika tamthilia teule, - kujadili uhalisia wa wahusika katika jamii yake, - kueleza uhusiano kati ya wahusika katika tamthilia teule, - kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake wa wahusika.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua dhamira, maudhui na wahusika katika tamthilia. - Kujiamini: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake uchambuzi wa dhamira, maudhui na wahusika. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochanganua maudhui, dhamira na wahusika katika tamthilia na kuwawasilishia wenzake.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapotambua na kujadili dhamira, maudhui na wahusika katika tamthilia. - Umoja: Mwanafunzi anapotagusana na wengine ili kutambua na kujadili dhamira, maudhui na wahusika katika tamthilia.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochanganua maudhui mbalimbali katika tamthilia.				

3.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
3.1 Fasihi Simulizi	3.1.1 Uchanganuzi wa Semi - Tanakali za sauti - Vitanzandimi - Vitendawili	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili katika fasihi simulizi ili kuzibainisha, - kufafanua sifa za tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili ili kuzipambanua, - kujadili umuhimu wa tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili katika jamii, - kutumia tanakali za sauti na vitendawili katika tungo, - kuwasilisha tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili,	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya tanakali za sauti, - kufafanua sifa za tanakali za sauti, - kutafiti mtandaoni umuhimu wa tanakali za sauti, - kujadili na wenzake umuhimu wa tanakali za sauti alizotafiti, - kutumia tanakali za sauti katika mazungumzo, - kueleza maana ya vitanzandimi, - kufafanua sifa za vitanzandimi, - kujadili umuhimu wa vitanzandimi, - kutunga vitanzandimi akishirikiana na wenzake, - kuwasilisha vitanzandimi alivyotunga kwa wenzake ili wavitathmini, - kueleza maana ya vitendawili,	Je, kuna uhusiano gani kati ya tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili?

		f) kufurahia matumizi ya tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili katika mawasiliano.	- kufafanua sifa za vitendawili, - kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu vitendawili, - kutega na kutegua vitendawili anavyofahamu akiwa na wenzake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili katika jamii. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotega na kutegua vitendawili. - Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilisha tungo zake kwa wenzake. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga vitanzandimi na kuwasilishia wenzake.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa tanakali za sauti, vitanzandimi na vitendawili katika jamii. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunga vitanzandimi. - Heshima: Mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu umuhimu wa vitendawili katika jamii.				
Masuala Mtambuko: - Usalama wa mtandaoni: Mwanafunzi anapotumia mtandao salama kusakura kuhusu umuhimu wa tanakali za sauti katika jamii. - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapotega na kutegua vitendawili kutoka jamii yake.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
3.2 Ushairi	3.2.1 Uchambuzi wa Mashairi - Maudhui - Dhamira	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kutambua maudhui na dhamira katika mashairi, - kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi ya diwani teule, - kutathmini uhusiano wa maudhui na dhamira katika mashairi ya diwani teule, - kuchangamkia uchambuzi wa mashairi katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi aelekezwe: - kusikiliza mashairi kutoka kwa kifaa cha kidijitali, mwenzake au mgeni mwalikwa ili kutambua ujumbe, - kusoma mashairi kutoka kwenye diwani teule ili kutambua maudhui na dhamira, - kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi ya diwani teule, - kutumia kifaa cha kidijitali kutafiti mashairi mbalimbali na kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi hayo, - kuwasambazia wenzake matokeo ya utafiti wake ili wayatathmini, - kujadili uhusiano wa maudhui na dhamira katika mashairi mbalimbali ya diwani teule.	- Mashairi huwasilisha ujumbe kuhusu mambo gani? - Kwa nini mtunzi hutunga mashairi?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilisha ipasavyo maudhui na dhamira katika mashairi mbalimbali. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu maana ya maudhui na dhamira.				

- Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni mashairi mbalimbali na kuchambua maudhui na dhamira. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua maudhui na dhamira katika mashairi ya diwani teule.
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapowasiliza wenzake na kuthamini michango yao katika kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi. - Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochambua maudhui na dhamira katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali alichokitumia.
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua mashairi mbalimbali.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
3.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	3.3.1 Uchambuzi wa Tamthilia <i>Mandhari</i> <i>Muundo</i> <i>Mtindo</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya mandhari, muundo na mtindo katika tamthilia, - kueleza umuhimu wa mandhari, muundo na mtindo katika tamthilia, - kubainisha vipengele vya mandhari, muundo na mtindo katika tamthilia teule, - kuchambua mandhari, muundo na mtindo katika tamthilia teule kwa kuzingatia vipengele vyake, - kuonea fahari uchambuzi wa mandhari, muundo na	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya mandhari katika tamthilia, - kubainisha vipengele vya mandhari (<i>wakati na mahali</i>), - kuchambua mandhari katika tamthilia teule kwa kuzingatia mahali na wakati wa matukio, - kujadili na wenzake maana ya muundo katika tamthilia, - kufanya utafiti mtandaoni na maktabani kuhusu vipengele vya muundo na kuwawasilishia wenzake ili wavitathmini, - kuchambua muundo katika tamthilia teule kwa kuzingatia vipengele vya muundo akiwa na wenzake, - kujadili na wenzake maana ya mtindo katika tamthilia, - kufanya utafiti mtandaoni na maktabani kuhusu vipengele vya mtindo na kuwawasilishia wenzake ili wavitathmini,	- Mahali na wakati unaorejelewa katika tamthilia huwa na umuhimu gani? - Ni nini kinachofanya tamthilia ivutie?

		mtindo katika tamthilia.	- kuchambua mtindo katika tamthilia teule kwa kuzingatia vipengele vya mtindo, - kuigiza na wenzake sehemu ya tamthilia teule.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake maana ya mandhari, muundo na mtindo katika tamthilia. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni au katika matini andishi maelezo kuhusu mandhari, muundo na mtindo. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kusoma maelezo kuhusu mandhari muundo na mtindo katika tamthilia.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua mandhari, muundo na mtindo katika tamthilia teule. - Heshima: Mwanafunzi anapotathmini maelezo ya wenzake kuhusu mandhari, muundo na mtindo huku akithamini mchango wa kila mmoja.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochanganua tamthilia.				

4.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
4.1 Fasihi Simulizi	4.1.1 Ushairi Simulizi Nyimbo • <i>Bembezezi</i> • <i>Nyimbo za watoto</i> • <i>Nyimbo za harusi</i> • <i>Nyimbo za dini</i> • <i>Nyimbo za siasa</i> • <i>Hodiya/ nyimbo za kazi</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya aina mbalimbali za nyimbo ili kuzipambanua, b) kutambua aina mbalimbali za nyimbo katika matini, c) kujadili nafasi ya aina mbalimbali za nyimbo, d) kufanya wasilisho la aina mbalimbali za nyimbo, e) kuchambua ujumbe katika aina mbalimbali za nyimbo, f) kuchanganua fani katika aina mbalimbali za nyimbo,	Mwanafunzi aelekezwe: • kueleza maana ya aina mbalimbali za nyimbo (<i>bembezezi, nyimbo za watoto, nyimbo za harusi, dini, siasa, hodiya – kimai na wawe</i>), • kutambua aina mbalimbali za nyimbo (<i>bembezezi, nyimbo za watoto, nyimbo za harusi, dini, siasa, hodiya – kimai na wawe</i>) katika matini mbalimbali, • kusakura mtandaoni na kubainisha aina mbalimbali za nyimbo, • kuwawasilishia wenzake aina mbalimbali za nyimbo ambazo alitafiti mtandaoni, • kujadili nafasi ya aina mbalimbali za nyimbo (<i>bembezezi, nyimbo za watoto, nyimbo za harusi, dini, siasa, hodiya – kimai na wawe</i>), • kujadili ujumbe katika aina mbalimbali za nyimbo (<i>bembezezi, nyimbo za watoto, nyimbo za</i>	Ni kwa namna gani aina mbalimbali za nyimbo huakisi tamaduni na maisha ya jamii husika?

		g) kuchangamkia aina mbalimbali za nyimbo katika jamii.	<i>harusi, dini, siasa, hodiya – kimai na wawe</i>), • kuwasilishia darasani aina mbalimbali za nyimbo, • kujadili fani katika aina mbalimbali za nyimbo (<i>bembezezi, nyimbo za watoto, nyimbo za harusi, dini, siasa, hodiya – kimai na wawe</i>), • kutafiti nyanjani kuhusu aina mbalimbali za nyimbo, • kuwawasilishia wenzake utafiti wake ili wautolee maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili nafasi ya aina mbalimbali za nyimbo. • Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilisha aina mbalimbali za nyimbo kwa wenzake. • Ubunifu: Mwanafunzi anapowasilisha aina mbalimbali za nyimbo. • Uraia: Mwanafunzi anapojadili umuhimu wa aina mbalimbali za nyimbo katika jamii yake.				
Maadili: • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa aina mbalimbali za nyimbo. • Heshima: Mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake wanapojadiliana.				
Masuala Mtambuko: • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapowasilisha aina mbalimbali za nyimbo. • Masuala ya elimu ya uraia: Mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu umuhimu wa aina mbalimbali za nyimbo. • Uongozi mwema: Mwanafunzi anapojadili nafasi ya nyimbo za kisiasa. • Elimu ya fedha: Mwanafunzi anapojadili kuhusu umuhimu wa nyimbo za kazi.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Liliopendekezwa
4.2 Ushairi	4.2.1 Uchambuzi wa Mashairi - Maudhui - Dhamira	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kutambua maudhui na dhamira katika mashairi, - kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi kwenye diwani teule, - kutathmini uhusiano wa maudhui na dhamira katika mashairi ya diwani teule, - kuchangamkia uchambuzi wa mashairi katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi aelekezwe: - kusoma mashairi mbalimbali ili kutambua maudhui na dhamira katika mashairi, - kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi ya diwani teule, - kutafiti mtandaoni mashairi mbalimbali na kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi hayo, - kuwasambazia wenzake matokeo ya utafiti wake ili wayatathmini, - kujadili uhusiano wa maudhui na dhamira katika mashairi mbalimbali katika diwani teule na mitandaoni.	Lengo la mashairi hutambulika vipi katika shairi?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Kujiamini: Mwanafunzi anapochambua ipasavyo maudhui na dhamira katika mashairi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposoma mashairi ili kuyachambua. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapojadili uhusiano wa maudhui na dhamira katika mashairi. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposoma na kuchambua maudhui na dhamira ya mashairi mtandaoni.				

Maadili: - Amani: Mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochambua maudhui na dhamira katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu maudhui na dhamira.
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua mashairi mbalimbali.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
4.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	4.3.1 Uchambuzi wa Riwaya <i>Maudhui</i> <i>Dhamira</i> <i>Wahusika</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya maudhui, dhamira na wahusika katika riwaya, b) kutambua maudhui, dhamira na wahusika katika riwaya teule, c) kuchambua maudhui, dhamira na wahusika katika riwaya teule, d) kuchangamkia usomaji na uchambuzi wa riwaya katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya maudhui katika riwaya, - kutambua maudhui katika riwaya teule, - kuchambua na wenzake maudhui mbalimbali katika riwaya teule, - kueleza maana ya dhamira katika riwaya, - kutambua dhamira katika riwaya teule, - kuchambua dhamira katika riwaya teule akiwa na mwenzake, - kueleza maana ya wahusika katika riwaya, - kutambua wahusika katika riwaya teule, - kujadili mambo yanayochangia uhusika katika riwaya, - kuchambua sifa za wahusika katika riwaya teule,	- Maudhui na dhamira huhusiana na kuathiriana vipi katika riwaya? - Ni nini humchochea mwandishi wa riwaya anapoteua wahusika wake?

			- kujadili mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika katika riwaya teule, - kujadili uhalisia wa wahusika wa riwaya katika jamii yake, - kuchanganua umuhimu wa wahusika katika riwaya teule.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapochanganua maudhui, dhamira na wahusika katika riwaya teule akiwa na wenzake. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kutafuta maana ya maudhui, dhamira na wahusika. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua maudhui, dhamira na wahusika katika riwaya teule. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kutafuta maana ya dhamira, maudhui na wahusika.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapochanganua maudhui, dhamira na wahusika katika riwaya teule. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili maudhui, dhamira na wahusika huku wakithamini maoni ya kila mmoja.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai kutegemea maudhui mbalimbali katika riwaya teule.				

5.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
5.1 Fasihi Simulizi	5.1.1 Uchanganuzi wa Mazungumzo - Mawaidha - Hotuba - Maapizo	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya mawaidha, hotuba na maapizo ili kuipambanua, - kutambua mawaidha, hotuba na maapizo katika matini, - kujadili umuhimu wa mawaidha, hotuba na maapizo katika jamii, - kuchambua ujumbe katika mawaidha, hotuba na maapizo, - kuchambua fani katika mawaidha, hotuba na maapizo, - kujadili mbinu za uwasilishaji wa mawaidha, hotuba na maapizo,	Mwanafunzi aelekezwe: - kusikiliza wasilisho la mawaidha, hotuba na maapizo kutoka kwa mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali, - kueleza maana ya mawaidha, hotuba na maapizo, - kutambua mawaidha, hotuba na maapizo katika matini, - kujadili umuhimu wa mawaidha, hotuba na maapizo, katika jamii, - kuchambua ujumbe katika mawaidha, hotuba na maapizo katika matini, - kuchambua fani katika mawaidha, hotuba na maapizo katika matini, - kujadili mbinu za uwasilishaji wa mawaidha, hotuba na maapizo,	- Je, ni kwa nini tunatoa mawaidha katika jamii? - Unazingatia nini unapowasilisha mawaidha, hotuba na maapizo?

		g) kuwasilisha mawaidha, hotuba na maapizo kwa kuzingatia mbinu zifaazo, h) kuchangamkia mawaidha, hotuba na maapizo katika jamii.	kuwasilisha mawaidha, hotuba na maapizo kwa kuzingatia mbinu zifaazo.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa mawaidha, hotuba na maapizo. - Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilisha mawaidha, hotuba na maapizo kwa wenzake. - Ubunifu: Mwanafunzi anapowasilisha mawaidha, hotuba na maapizo. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua ujumbe na fani katika mawaidha, hotuba na maapizo.				
Maadili: - Heshima: Mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake wanapojadiliana. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili nafasi ya mawaidha, hotuba na maapizo.				
Masuala Mtambuko: - Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake mawaidha, hotuba na maapizo. - Masuala ya elimu ya uraia: Mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu umuhimu wa mawaidha, hotuba na maapizo katika jamii.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
5.2 Ushairi	5.2.1 Uchambuzi wa Mashairi - Mandhari - Wahusika	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kutambua mandhari katika mashairi, - kujadili umuhimu wa mandhari katika shairi, - kutambua wahusika katika shairi, - kujadili umuhimu wa wahusika katika mashairi, - kuchambua mandhari na wahusika katika mashairi ya diwani teule, - kuchangamkia matumizi ya mandhari na wahusika katika mashairi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutambua mandhari (<i>mahali na wakati</i>) katika mashairi kwenye diwani teule, - kujadili umuhimu wa mandhari (<i>mahali na wakati</i>) katika mashairi kwenye diwani teule au mtandaoni, - kuchambua mandhari katika mashairi ya diwani teule akizingatia mahali na wakati, - kuwasilisha uchambuzi wake wa mandhari kwa wenzake. - kutambua wahusika (<i>nafsineni na nafsinenewa</i>) katika mashairi mbalimbali ya diwani teule, - kujadili umuhimu wa wahusika (<i>nafsineni na nafsinenewa</i>) aliotambua katika mashairi,	- Ni aina gani za mandhari unazozijua kutokana na mashairi uliyowahi kusoma? - Kwa nini mtunzi wa mashairi hutumia wahusika katika uandishi wa mashairi?

			- kuchambua wahusika (<i>nafsineni na nafsinenewa</i>) katika mashairi ya diwani teule, - kuwasilisha uchambuzi wake wa wahusika kwa wenzake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilisha uchambuzi wa mandhari na wahusika katika ushairi. - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake umuhimu wa mandhari. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua mandhari na wahusika katika mashairi.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua wahusika na mandhari. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochambua wahusika na mandhari katika mashairi na kuwasilishia wenzake uchambuzi wake. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu wahusika na mandhari.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua mashairi mbalimbali.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
5.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	5.3.1 Uchambuzi wa Riwaya <i>Mandhari</i> <i>Muundo</i> <i>Mtindo</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya mandhari, muundo na mtindo katika riwaya, - kutambua mandhari, muundo na mtindo katika riwaya teule, - kuchambua mandhari, muundo na mtindo katika riwaya teule, - kuchanganua umuhimu wa mandhari, muundo na mtindo katika riwaya teule, - kujenga mazoea ya usomaji wa kazi za kifasihi katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza dhana ya mandhari katika riwaya kwa kuzingatia mahali pa tukio, wakati na hali, - kueleza umuhimu wa mandhari katika riwaya teule, - kuchambua mandhari katika riwaya teule, - kufanya utafiti mtandaoni na kwenye matini andishi kuhusu vipengele vya muundo na kuwawasilishia wenzake, - kueleza maana ya muundo katika riwaya, - kueleza umuhimu wa muundo katika riwaya, - kuchambua vipengele vya muundo katika riwaya teule akiwa na wenzake, - kueleza maana ya mtindo katika riwaya, - kueleza umuhimu wa mtindo katika riwaya,	- Mahali na wakati unaorejelewa katika riwaya huwa na umuhimu gani? - Riwaya hutambuliwa vipi kimuundo? - Mtindo huchangia vipi mvuto katika riwaya?

			kuchambua vipengele vya mtindo katika riwaya teule akiwa na wenzake.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili vipengele vya muundo na mtindo wa riwaya teule akiwa na wenzake. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo wa riwaya. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni au katika matini andishi ili kupata maelezo kuhusu mandhari, muundo na mtindo.				
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapofanya utafiti kwa kusakura mtandao salama ili kupata maelezo ya mandhari, muundo na mtindo. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya. - Heshima: Mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu vipengele vya muundo na mtindo huku akithamini maoni ya kila mmoja.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua riwaya.				

6.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
6.1 Fasihi Simulizi	6.1.1 Uchanganuzi wa Maigizo • <i>Michezo ya jukwaani</i> • <i>Vichekesho</i> • <i>Michezo ya watoto</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto katika utanzu wa maigizo, b) kufafanua sifa za michezo ya jukwaani, vichekesho, michezo ya watoto ili kuzipambanua, c) kujadili umuhimu wa michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto katika jamii, d) kujadili vipengele vya uwasilishaji wa michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto ili kuvitambulisha,	Mwanafunzi aelekezwe: • kutafiti mtandaoni maana ya michezo ya jukwaani, • kujadili na wenzake maana ya michezo ya jukwaani, • kutazama video kuhusu michezo ya jukwaani na kutambua sifa za michezo ya jukwaani, • kufafanua sifa za michezo ya jukwaani kutokana na video aliyotazama, • kujadili na wenzake umuhimu wa michezo ya jukwaani katika jamii, • kujadili vipengele vya uwasilishaji wa michezo ya jukwaani, • kuigiza michezo ya jukwaani kwa kuzingatia vipengele vifaavyo, • kueleza maana ya vichekesho, • kufafanua sifa za vichekesho, • kujadili na wenzake umuhimu wa vichekesho katika jamii, • kujadili vipengele vya uwasilishaji wa vichekesho,	Je, ni mambo yapi hutambulisha na kutofautisha michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto?

		e) kuwasilisha michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto kwa kuzingatia vipengele vifaavyo, f) kuonea fahari uwasilishaji wa michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto katika jamii.	• kuwasilisha vichekesho kwa kuzingatia vipengele vifaavyo, • kueleza maana michezo ya watoto, • kujadili na wenzake sifa za michezo ya watoto, • kujadili na wenzake umuhimu wa michezo ya watoto katika jamii, • kujadili vipengele vya uwasilishaji wa michezo ya watoto, • kuigiza michezo ya watoto kwa kuzingatia vipengele vifaavyo.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto. • Ubunifu: Mwanafunzi anapowasilisha michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto. • Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilisha michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto. • Uraia: Mwanafunzi anapowasilisha michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto kutoka jamii yake.				
Maadili: • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto. • Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili umuhimu wa michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto kutoka jamii yake. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapoigiza michezo ya jukwaani na michezo ya watoto.				

Masuala Mtambuko:

- Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto kutoka kwa jamii yake.
- Uraia: Mwanafunzi anapowasilisha michezo ya jukwaani, vichekesho na michezo ya watoto kutoka jamii yake.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
6.2 Ushairi	6.2.1 Uchambuzi wa Mashairi ya Arudhi <i>Muundo</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza vipengele vya muundo wa mashairi ya arudhi, b) kutambua vipengele vya muundo wa mashairi ya arudhi katika diwani teule, c) kuchambua mashairi ya arudhi kimuundo katika diwani teule, d) kufurahia uchambuzi wa vipengele vya muundo katika mashairi arudhi.	Mwanafunzi aelekezwe: • kutafiti vitabuni na mtandaoni kuhusu vipengele vya muundo wa mashairi ya arudhi, • kueleza vipengele vya muundo wa mashairi ya arudhi kutokana na utafiti wake, • kutambua vipengele vya muundo wa mashairi ya arudhi katika diwani teule, • kuchambua mashairi ya arudhi ya diwani teule kimuundo, • kuwasilisha uchambuzi wa mashairi ya arudhi kwa wenzake ili wautathmini.	1. Ni vipengele gani vya kimuundo vinavyozingatiwa katika uchambuzi wa mashairi ya arudhi? 2. Vipengele vya muundo vinatofautishaje mashairi mbalimbali ya arudhi?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake uchambuzi wa mashairi ya arudhi. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua mashairi ya arudhi kwa kuzingatia muundo wake. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu vipengele vya muundo vya mashairi ya arudhi. • Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilishia wenzake uchambuzi wa mashairi ya arudhi kimuundo.				

Maadili: • Umoja: Mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua mashairi ya arudhi kimuundo. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotafiti kuhusu uchambuzi wa mashairi mtandaoni na kutunza kifaa cha kidijitali anachotumia. • Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapowasilisha uchambuzi wa mashairi ya arudhi kimuundo.
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua mashairi mbalimbali katika diwani teule.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
6.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	6.3.1 Uchambuzi wa Wasifu • <i>Maudhui</i> • <i>Dhamira</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya wasifu ili kuipambanua, b) kueleza umuhimu wa wasifu katika jamii, c) kutambua maudhui na dhamira katika wasifu teule, d) kuchambua maudhui na dhamira katika wasifu teule, e) kuchangamkia usomaji wa wasifu ili kujiendeleza maishani.	Mwanafunzi aelekezwe: • kutafiti mtandaoni au katika matini andishi maana ya wasifu, • kueleza maana ya wasifu kutokana na utafiti wake, • kueleza umuhimu wa wasifu katika jamii, • kutambua maudhui katika wasifu teule, • kuchambua maudhui katika wasifu teule, • kutambua dhamira katika wasifu teule, • kuchambua dhamira katika wasifu teule, • kujadili umuhimu wa wasifu teule kwa kutathmini mafunzo na maadili yanayowasilishwa katika wasifu, • kutafiti mtandaoni au maktabani kazi za wasifu na kuchambua maudhui na dhamira.	Ni matendo gani ya mtu yanayoweza kumchochea mwandishi kuandika wasifu kuhusu mtu huyo?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapochanganua maudhui na dhamira katika wasifu teule akiwa na wenzake. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kutafuta maana ya wasifu. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua maudhui na dhamira katika wasifu teule. • Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni au maktabani kujifunza maana ya wasifu.
Maadili: • Heshima: Mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapochanganua maudhui na dhamira katika wasifu teule. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya uchambuzi wa maudhui na dhamira. • Amani: Mwanafunzi anapojadili na wenzake kwa utulivu umuhimu wa wasifu.
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai kutegemea maudhui katika wasifu teule.

7.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
7.1 Fasihi Simulizi	7.1.1 Uchanganuzi wa Hadithi • Tarihi • Kumbukumbu	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya tarihi na kumbukumbu ili kuzipambanua, b) kutambua tarihi na kumbukumbu katika matini, c) kueleza umuhimu wa tarihi na kumbukumbu katika jamii, d) kuchambua ujumbe na fani katika tarihi na kumbukumbu, e) kujadili mbinu za uwasilishaji wa tarihi na kumbukumbu, f) kufanya wasilisho la tarihi na kumbukumbu,	Mwanafunzi aelekezwe: • kutafiti mtandaoni au maktabani maana ya tarihi na kumbukumbu, • kueleza maana ya tarihi na kumbukumbu kutokana na utafiti wake, • kutambua tarihi na kumbukumbu katika matini, • kueleza umuhimu wa tarihi na kumbukumbu katika jamii, • kusakura mtandaoni ili kusikiliza na/au kutazama tarihi na kumbukumbu, • kutambua ujumbe na fani kutoka matini alizozisikiliza au kutazama mtandaoni, • kuchambua ujumbe na fani katika tarihi na kumbukumbu, • kumsikiliza mgeni mwalikwa akiwasilisha tarihi na	1. Ni matukio gani yanayoweza kuandikiwa tarihi katika jamii? 2. Je, kumbukumbu uliyowahi kusimuliwa ilikuwa na ujumbe gani?

		g) kufurahia tarihi na kumbukumbu katika jamii.	kumbukumbu ili kupata mbinu za uwasilishaji, • kujadili mbinu za uwasilishaji wa tarihi na kumbukumbu kutokana na tarihi na kumbukumbu alizozisikiliza, • kufanya wasilisho la tarihi na kumbukumbu akizingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa tarihi na kumbukumbu. • Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilisha tarihi na kumbukumbu kwa wenzake. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni maana ya tarihi na kumbukumbu. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua ujumbe katika tarihi na kumbukumbu.				
Maadili • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa tarihi na kumbukumbu. • Uadilifu: Mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake wanapojadiliana. • Uzalendo: Mwanafunzi anapowasilisha tarihi na kumbukumbu kuhusu nchi yake.				
Masuala Mtambuko: • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapothamini tarihi na kumbukumbu za jamii yake na jamii nyingine. • Masuala ya elimu ya uraia: Mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu nafasi ya tarihi na kumbukumbu katika jamii.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
7.2 Ushairi	7.2.1 Uchambuzi wa Mashairi Mtindo • <i>Nidaa</i> • <i>Maswali balagha</i> • <i>Methali</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya nidaa, maswali balagha na methali katika ushairi, b) kufafanua umuhimu wa nidaa, maswali balagha na methali katika ushairi, c) kutambua nidaa, maswali balagha na methali katika mashairi kwenye diwani teule, d) kuchanganua matumizi ya nidaa, maswali balagha na methali katika mashairi kwenye diwani teule, e) kufurahia matumizi ya nidaa, maswali balagha na methali katika mashairi.	Mwanafunzi aelekezwe: • kueleza maana ya nidaa, maswali balagha na methali, • kutafiti mtandaoni au vitabuni umuhimu wa nidaa, maswali balagha na methali katika ushairi, • kufafanua umuhimu wa nidaa, maswali balagha na methali katika ushairi kutokana na utafiti wake, • kughani au kusoma mashairi katika diwani teule, • kutambua nidaa, maswali balagha na methali katika mashairi kwenye diwani teule, • kuchanganua matumizi ya nidaa, maswali balagha na methali katika mashairi kwenye diwani teule na kuwasilishia wenzake.	1. Ni vipi ambavyo hisia mbalimbali zinaweza kuwasilishwa katika shairi? 2. Ni vipengele gani vya mtindo unavyovijua?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapochambua na wenzake matumizi ya nidaa, maswali balagha na methali. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti kuhusu nidaa, maswali balagha na methali mitandaoni. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua nidaa, maswali balagha na methali katika mashairi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata umuhimu wa nidaa, maswali balagha na methali.
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua nidaa, maswali balagha na methali katika shairi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochambua nidaa, maswali balagha na methali katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali anachotumia. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu nidaa, maswali balagha na methali.
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko mbalimbali katika mashairi katika diwani teule.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
7.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	7.3.1 Uchambuzi wa Wasifu <i>Wahusika</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua wahusika katika wasifu teule, b) kuchambua sifa za wahusika katika wasifu teule, c) kutathmini maadili yanayotokana na maisha ya mhusika mkuu katika wasifu teule, d) kuchangamkia usomaji wa wasifu ili kujiendeleza maishani.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutambua wahusika kwa kusoma wasifu teule, - kuchambua sifa za wahusika katika wasifu teule, - kutambua mhusika mkuu katika wasifu teule, - kuchambua maisha ya mhusika mkuu na maadili yanayokuzwa kupitia maisha yake katika wasifu teule, - kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu maisha ya mhusika mkuu na maadili yanayokuzwa, - kujadili uhalisia wa mhusika wa wasifu teule katika jamii yake.	Ni mchango gani katika jamii unaoweza kumfanya mhusika kuandikiwa wasifu?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapoeleza wenzake kuhusu wahusika katika wasifu. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anaposoma wasifu ili kujifunza maadili yanayotokana na mhusika mkuu. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua wahusika katika wasifu teule. - Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilishia wenzake uchambuzi wake kuhusu maisha ya mhusika mkuu na maadili yanayokuzwa.				

Maadili:

- Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua wahusika katika wasifu teule.
- Heshima: Mwanafunzi anapotathmini maelezo ya wenzake kuhusu wahusika huku akithamini mchango wa kila mmoja.
- Haki za kijamii: Mwanafunzi anapojadili uhalisia wa mhusika mkuu wa wasifu teule katika jamii yake akizingatia maadili ya jamii.
- Uzalendo: Mwanafunzi anapojadili kuhusu mhusika mkuu katika wasifu na mchango wake katika taifa.

Masuala Mtambuko:

Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anaposoma wasifu na kuchambua wahusika.

8.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
8.1 Fasihi Simulizi	8.1.1 Uchanganuzi wa Semi • Lakabu • Misimu	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya lakabu na misimu ili kuzipambanua, - kufafanua sifa za lakabu na misimu kama tungo za fasihi simulizi, - kujadili umuhimu wa lakabu na misimu kama tungo za fasihi simulizi, - kutumia lakabu na misimu katika tungo za fasihi simulizi, - kuchangamkia matumizi ya lakabu na misimu katika tungo za fasihi simulizi.	Mwanafunzi aelekezwe: • kueleza maana ya lakabu na misimu, • kutambua lakabu na misimu kwenye tungo za fasihi simulizi, • kusikiliza lakabu na misimu katika kifaa cha kidijitali, • kutambua sifa za lakabu na misimu alizosikiliza katika kifaa cha kidijitali, • kufafanua sifa za lakabu na misimu kama tungo za fasihi simulizi, • kutafiti mtandaoni au maktabani umuhimu wa lakabu na misimu, • kujadili na wenzake umuhimu wa lakabu na misimu,	Unajua lakabu na misimu gani katika jamii yako?

			kushirikiana na wenzake kuwasilisha tungo zilizotumia lakabu na misimu.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa lakabu na misimu. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu lakabu na misimu. - Uraia: Mwanafunzi anapojifunza umuhimu wa lakabu na misimu katika jamii yake. - Ubunifu: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuwasilisha tungo zilizotumia lakabu na misimu.				
Maadili: - Uzalendo: Mwanafunzi anapoeleza matumizi ya lakabu na misimu katika jamii yake. - Upendo: Mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi kushiriki katika shughuli za ujifunzaji. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.				
Masuala Mtambuko: Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapozingatia usalama wake anaposakura mtandaoni kuhusu lakabu na misimu.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
8.2 Ushairi	8.2.1 Uchambuzi wa Mashairi Mtindo <i>Usambamba</i> <i>Takriri</i> <i>Tabaini</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya usambamba, takriri na tabaini ili kuzipambanua, - kufafanua umuhimu wa usambamba, takriri na tabaini katika ushairi, - kutambua usambamba, takriri na tabaini katika mashairi kwenye diwani teule, - kuchanganua matumizi ya usambamba, takriri na tabaini katika mashairi kwenye diwani teule, - kufurahia matumizi ya usambamba, takriri na tabaini katika mashairi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti mtandaoni au maktabani maana ya usambamba, takriri na tabaini, - kueleza maana ya usambamba, takriri na tabaini kutokana na utafiti wake, - kutafiti mtandaoni au vitabuni umuhimu wa usambamba, takriri na tabaini katika ushairi, - kujadili na wenzake matokeo ya utafiti wake ili wayatathmini, - kughani mashairi kwa kuzingatia mahadhi mbalimbali, - kutambua usambamba, takriri na tabaini kwa kurejelea mashairi kwenye diwani teule, - kuchanganua matumizi ya usambamba, takriri na tabaini katika mashairi kwenye diwani teule, - kuchanganua matumizi ya usambamba, takriri na tabaini	Ni kwa nini mtunzi wa mashairi hutumia mbinu mbalimbali za kimtindo katika mashairi anayotunga?

			kwa kurejelea mashairi mengine mtandaoni au maktabani.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapochambua na wenzake matumizi ya usambamba, takriri na tabaini. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti kuhusu usambamba, takriri na tabaini mtandaoni. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua usambamba, takriri na tabaini katika mashairi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata umuhimu wa usambamba, takriri na tabaini.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua usambamba, takriri na tabaini. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochambua usambamba, takriri na tabaini katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali. - Uadilifu: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu usambamba, takriri na tabaini.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua mashairi mbalimbali katika diwani teule.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
8.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	8.3.1 Uchambuzi wa Hadithi fupi <i>Maudhui</i> <i>Dhamira</i> <i>Wahusika</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi, - kutambua maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi teule, - kuchambua maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi teule, - kuchangamkia uchambuzi wa maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi, - kusoma hadithi fupi teule na kutambua maudhui, dhamira na wahusika mbalimbali, - kuchambua maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi teule, - kuwawasilishia wenzake uchambuzi wake kuhusu maudhui, dhamira na wahusika, - kujadili usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule, - kuchanganua umuhimu wa wahusika katika hadithi fupi teule, - kujadili uhalisia wa wahusika wa hadithi fupi katika jamii yake, - kutazama hadithi fupi zinazowasilishwa kimaigizo katika vifaa vya kidijitali na kuzichambua kwa kuzingatia maudhui, dhamira na wahusika.	Je, wahusika huchangia vipi maudhui na dhamira katika hadithi fupi?

Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi teule. - Uraia: Mwanafunzi anapojadili uhalisia wa wahusika wa hadithi fupi katika jamii yake. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapochambua maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi teule. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapotazama hadithi fupi zilizowasilishwa kimaigizo na kuchambua maudhui, dhamira na wahusika.
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi teule. - Heshima: Mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu maudhui, dhamira na wahusika katika hadithi fupi huku akithamini maoni ya kila mmoja. - Amani: Mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake wanapojadili uhalisia wa wahusika katika jamii. - Haki za kijamii: Mwanafunzi wanapojadili uhalisia wa wahusika katika jamii kwa uadilifu.
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochanganua maudhui mbalimbali katika hadithi fupi.

9.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
9.1 Fasihi Simulizi	9.1.1 Uchanganuzi wa Ushairi Simulizi Maghani simulizi: - Rara - Rara nafsi - Tendi/tenzi	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza maana ya maghani simulizi kama kipera cha ushairi simulizi, - kufafanua sifa za maghani simulizi ili kuzipambanua, - kujadili umuhimu wa maghani simulizi katika jamii, - kueleza maana ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi kama aina za maghani simulizi, - kueleza sifa za rara, rara nafsi na tendi/tenzi kama aina za maghani simulizi,	Mwanafunzi aelekezwe: - kutumia kamusi au mtandao salama kutafuta maana ya maghani simulizi, - kueleza maana ya maghani simulizi kutokana na utafiti wake, - kutumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu sifa za maghani simulizi, - kujadili na wenzake kuhusu sifa za maghani simulizi, - kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa maghani simulizi katika jamii, - kusoma vielelezo vya rara, rara nafsi na tendi/tenzi ili kutambua maana za aina hizo za maghani simulizi, - kueleza maana ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi kutokana na vielelezo alivyosoma,	- Je, unafahamu mashairi gani yanayozungumzi a kuhusu watu mashuhuri? - Maghani simulizi yanatofautiana vipi na maghani ya kawaida?

		f) kujadili umuhimu wa rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii, g) kuchanganua rara, rara nafsi na tendi/tenzi kwa kuzingatia maudhui na fani, h) kufurahia matumizi ya maghani simulizi katika miktadha mbalimbali ya kijamii.	• kusakura mtandaoni au kutafiti katika matini andishi kuhusu sifa za rara, rara nafsi na tendi/tenzi kama aina za maghani simulizi, • kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatolee maoni, • kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii, • kutafiti kuhusu rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii yake na kuwasilishia wenzake matokeo ya utafiti wake, • kueleza vipengele vya rara, rara nafsi na tendi/tenzi kama aina za maghani simulizi, • kuchanganua vipengele vya rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika matini, • kutafiti matumizi ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii zao na kuandika ripoti ya utafiti wake,	
--	--	--	--	--

			• kuwasilisha ripoti ya utafiti wake kwa wenzake ili watoe maoni yao, • kutunga rara, rara nafsi na tendi/tenzi na kuwasilishia wenzake ili wamtotee maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: • Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa maghani simulizi katika jamii. • Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni sifa za rara, rara nafsi na tendi/tenzi. • Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi. • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochanganua vipengele vya rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika matini. • Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga rara, rara nafsi na tendi/tenzi.				
Maadili: • Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu umuhimu wa rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii. • Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii yake. • Uwajibikaji: Mwanafunzi anaposhiriki katika utafiti kuhusu matumizi ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii yake. • Amani: Mwanafunzi anapotangamana na watu katika jamii yake anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii.				
Masuala Mtambuko: • Mshikamano wa kijamii: Mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii yake. • Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapotumia mtandao salama katika utafiti kuhusu sifa za maghani simulizi. • Uraia: Mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya rara, rara nafsi na tendi/tenzi katika jamii yake.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
9.2 Ushairi	9.2.1 Uchambuzi wa Mashairi - Mistari katika shairi (Aina za mistari - Uamilifu/utendakazi) - Toni - Mazaji	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza aina za mistari katika ushairi, - kutambua aina za mistari katika shairi, - kuchambua matumizi ya aina za mistari katika mashairi, - kueleza maana ya toni na mazaji katika mashairi, - kueleza aina za toni na mazaji katika mashairi, - kutambua aina za toni na mazaji katika mashairi, - kuchambua matumizi ya toni na mazaji katika mashairi, - kufurahia matumizi ya mistari, toni na mazaji katika mashairi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza aina za mistari katika ushairi (<i>k.v. mistari kifu, mistari mishata, mistari wazi n.k.</i>) - kusoma mashairi mbalimbali ili kutambua aina za mistari, - kutambua aina za mistari katika mashairi kwenye diwani teule, - kutafiti mitandaoni kuhusu matumizi ya aina za mistari katika mashairi, - kujadili uamilifu wa aina za mistari katika mashairi kwenye diwani teule, - kuchambua matumizi ya mistari katika mashairi mbalimbali, - kueleza maana ya toni na mazaji, - kueleza aina za toni na mazaji katika mashairi ya diwani teule, - kutafiti mtandaoni umuhimu wa toni na mazaji katika mashairi,	- Mistari katika mashairi huchangia vipi umbo la shairi? - Ni toni gani unazoweza kutambua kutokana na mashairi mbalimbali uliyosoma? - Je, ni kwa jinsi gani mpangilio wa mistari katika shairi huathiri uwasilishaji wa hisia?

			- kughani mashairi kwa kuzingatia toni faafu. - kuchambua matumizi ya toni na mazaji katika diwani teule na kuwasilisha majibu yake kwa wenzake ili wayatolee maoni.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa aina za mistari, toni na mazaji katika mashairi. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu aina za mistari, toni na mazaji. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu aina za mistari katika mashairi, toni na mazaji. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapochambua matumizi ya toni na mazaji katika diwani teule.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua aina za mistari. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapochambua matumizi ya mistari katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali. - Upendo: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua matumizi ya toni na mazaji katika diwani teule.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua mashairi mbalimbali katika diwani teule.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
9.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	9.3.1 Uchambuzi wa Hadithi Fupi <i>Mandhari</i> <i>Muundo</i> <i>Mtindo</i>	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kutambua mandhari, vipengele vya muundo na mtindo katika hadithi fupi teule, - kuchambua mandhari, vipengele vya muundo na mtindo katika hadithi fupi teule, - kutathmini umuhimu wa mandhari, vipengele vya muundo na mtindo katika hadithi fupi teule, - kuonea fahari nafasi ya mandhari, muundo na mtindo katika hadithi fupi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kueleza maana ya mandhari katika hadithi fupi, - kubainisha vipengele vya mandhari (<i>wakati na mahali</i>), - kuchambua mandhari katika hadithi fupi teule kwa kuzingatia mahali na wakati wa matukio, - kujadili na wenzake maana ya muundo katika hadithi fupi, - kufanya utafiti mtandaoni na maktabani kuhusu vipengele vya muundo na kuwawasilishia wenzake ili wavitathmini, - kuchambua muundo katika hadithi fupi teule kwa kuzingatia vipengele vya muundo akiwa na wenzake, - kujadili na wenzake maana ya mtindo katika hadithi fupi, - kufanya utafiti mtandaoni na maktabani kuhusu vipengele vya	- Mandhari ya hadithi huchangia vipi uhalisia wa matukio? - Kwa nini hadithi fupi mbalimbali huwa na mtindo tofautitofauti?

55

			mtindo na kuwawasilishia wenzake ili wavitathmini, - kuchambua mtindo katika hadithi fupi teule kwa kuzingatia vipengele vya mtindo, - kuigiza na wenzake sehemu ya hadithi fupi teule.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadili na wenzake mandhari na vipengele vya muundo na mtindo katika hadithi fupi teule. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu vipengele vya muundo na mtindo wa hadithi. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo. - Uwazaji kina na utatuzi: Mwanafunzi anapochambua mandhari, vipengele vya muundo na mtindo katika diwani teule. - Kujiamini: Mwanafunzi anapowawasilishia wenzake kwa ujasiri matokeo ya utafiti wake kuhusu vipengele vya muundo na mtindo.				
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapofanya utafiti kwa kusakura mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika hadithi fupi teule. - Heshima: Mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake kuhusu vipengele vya muundo na mtindo.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai mwanafunzi anapochambua hadithi fupi.				

56

10.0				
Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa
10.1 Fasihi Simulizi	10.1.1 Utafiti katika Fasihi Simulizi - Hatua za ukusanyaji data - Mbinu za ukusanyaji data - Mbinu za kurekodi na kuhifadhi data	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza hatua na mbinu za ukusanyaji data katika utafiti wa fasihi simulizi, - kujadili mbinu za kurekodi na kuhifadhi data katika utafiti wa fasihi simulizi, - kufafanua ufaafu na udhaifu wa mbinu mbalimbali za kurekodi na kuhifadhi data, - kufanya utafiti akizingatia hatua zifaazo, mbinu za ukusanyaji data zifaazo na mbinu mwafaka za kurekodi na kuhifadhi data, - kuthamini ukusanyaji na kuhifadhi wa data katika utafiti wa fasihi simulizi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti mtandaoni au maktabani kuhusu hatua na mbinu za ukusanyaji data, - kueleza wenzake hatua za ukusanyaji data kutokana na utafiti wake, - kuwaeleza wenzake mbinu za ukusanyaji data kutokana na utafiti wake, - kujadili mbinu za kurekodi na kuhifadhi data, - kufafanua ufaafu na udhaifu wa mbinu mbalimbali za kurekodi na kuhifadhi data, - kuteua mada ya fasihi simulizi ya kufanyia utafiti, - kufanya utafiti wa kiwango chake akizingatia hatua zifaazo, mbinu za ukusanyaji data zifaazo na	- Kwa nini utafiti wa fasihi simulizi huhitajika? - Ni utaratibu gani unaofaa kuzingatiwa katika kufanya utafiti?

			mbinu mwafaka za kurekodi na kuhifadhi data.	
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu ukusanyaji wa data katika utafiti wa fasihi simulizi. - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapowaeleza wenzake kuhusu mbinu za ukusanyaji wa data. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapofafanua ufaafu na udhaifu wa mbinu mbalimbali za kurekodi na kuhifadhi data. - Ubunifu: Mwanafunzi anapoteua mada atakayofanyia utafiti.				
Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kueleza kuhusu ukusanyaji na kuhifadhi wa data katika utafiti wa fasihi simulizi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotafiti katika mtandao salama au maktabani kuhusu hatua na mbinu za ukusanyaji data. - Haki za kijamii: Mwanafunzi anapoheshimu tamaduni za jamii anazotangamana nazo katika kufanya utafiti wake. - Kujiamini: Mwanafunzi anapowaeleza wenzake mbinu za ukusanyaji data kutokana na utafiti wake.				
Masuala Mtambuko: Masuala mtambuko anuwai kutokana na masuala ya utafiti.				

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Liliopendekezwa
10.2 Ushairi	10.2.1 Utunzi wa Mashairi ya Arudhi	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kujadili hatua za utunzi wa mashairi ya arudhi, - kutunga shairi la arudhi kwa kuzingatia hatua za utunzi zifaazo, - kuonea fahari utunzi wa mashairi ya arudhi.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti mtandaoni au maktabani kuhusu hatua zinazozingatiwa katika utunzi wa mashairi ya arudhi, - kujadili na wenzake hatua za utunzi wa mashairi ya arudhi (<i>k.v. maandalizi tangulizi, nakala ya kwanza, uhariri, nakala safi, uchapishaji</i>), kuibua mawazo (<i>k.v mada, dhamira, maudhui, nafsini, nafsini, mtindo, muundo</i>), kuandika nakala ya kwanza, kuhariri kazi aliyoundika, kuandika nakala safi ya kazi aliyohariri, - kutunga shairi la arudhi kwa kuzingatia hatua za utunzi zifaazo, - kuwasambazia wenzake kazi yake mtandaoni au kuwasomea ili waitolee maoni.	Je, unazingatia nini unapotunga mashairi ya arudhi?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu hatua za utunzi wa mashairi ya arudhi. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga shairi la arudhi kwa kuzingatia hatua zifaazo za utunzi wa mashairi. - Kujiamini: Mwanafunzi anapotunga na kuwasambazia wenzake kazi yake ili waitolee maoni.				

Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapowasambazia shairi la arudhi alilotunga mtandaoni ili waitolee maoni.
Maadili: - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapoandika na kuwasambazia wenzake kazi yake ili waitathmini. - Umoja: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili hatua za uandishi wa mashairi ya arudhi. - Heshima: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu hatua za uandishi wa mashairi ya arudhi na kuthamini maoni yao.
Masuala Mtambuko: Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapotafiti katika mtandao salama kuhusu hatua za utunzi wa mashairi ya arudhi.

Mada	Mada Ndogo	Matokeo Maalum Yanayotarajiwa	Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa	Swali Dadisi Lililopendekezwa
10.3 Bunilizi na Kazi za Kihalisia	10.3.1 Utunzi wa Bunilizi na Kazi za Kihalisia	Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: - kueleza sifa za mwandishi bora wa bunilizi na kazi za kihalisia, - kuandika bunilizi fupi au wasifu akizingatia hatua zifaazo, - kuonea fahari utunzi wa bunilizi na kazi za kihalisia katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi aelekezwe: - kutafiti mtandaoni au maktabani kuhusu sifa za mwandishi bora wa bunilizi na kazi za kihalisia, - kujadili na wenzake sifa za mwandishi bora wa bunilizi na kazi za kihalisia, - kufafanua jinsi ya kupata maudhui ya kuandikia bunilizi na kazi za kihalisia, - kutambua watu katika jamii ambao wasifu unaweza kuandikwa kuwahusu, - kuandika bunilizi fupi (<i>k.v. sura moja ya riwaya, onyesho la tamthilia au hadithi fupi moja</i>) au wasifu kuhusu maisha ya mtu.	Je, unapoandika kazi za kubuni na za kihalisia utapataje ujumbe unaoandikia?
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa: - Kujiamini: Mwanafunzi anapowasilishia wenzake sifa za mwandishi bora wa fasihi bunilizi na kazi za kihalisia. - Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili sifa za mwandishi bora. - Ujuzi wa kidijitali: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu sifa za mwandishi bora. - Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu sifa za mwandishi bora wa fasihi bunilizi. - Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: Mwanafunzi anapoibua maudhui ya kuandikia bunilizi au kazi ya kihalisia. - Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga bunilizi au kazi ya kihalisia.				

Maadili: - Umoja: Mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake anapowawasilishia sifa za mwandishi bora wa bunilizi. - Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu sifa za mwandishi bora wa bunilizi. - Heshima: Mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake.
Masuala Mtambuko: Usalama mtandaoni: Mwanafunzi anapotafiti kuhusu bunilizi kwa kurejelea mtandao salama.

VIGEZO NA VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHMINI**FASIHI SIMULIZI**

Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kuchambua hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua kwa kina hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.	Anachambua baadhi ya hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.
Kuweza kuchanganua semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachanganua kwa utondoti semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachanganua semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachanganua semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.	Anachanganua baadhi ya semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.
Kuweza kuchambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua kwa uketo maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.	Anachambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake kwa kuongozwa.
Kuweza kuchanganua	Anachanganua kwa utondoti mashairi	Anachanganua mashairi simulizi kwa	Anachanganua mashairi simulizi	Anachanganua baadhi ya mashairi simulizi kwa

63

Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
mashairi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	kuzingatia vipengele vyake.	kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.	kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.
Kuweza kuchambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua kwa kina mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake.	Anachambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake.	Anachambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake kwa kusaidiwa.

64

USHAIRI

Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kuainisha mashairi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya uainishaji.	Anaainisha kwa wepesi mashairi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya uainishaji.	Anaainisha mashairi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya uainishaji.	Anaainisha baadhi ya mashairi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya uainishaji.	Anaainisha baadhi ya mashairi kwa kuzingatia baadhi ya vigezo vya uainishaji.
Kuweza kuchambua mashairi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ushairi.	Anachambua kwa kina mashairi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ushairi.	Anachambua mashairi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ushairi.	Anachambua baadhi ya mashairi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ushairi.	Anachambua baadhi ya mashairi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya ushairi.
Kuweza kutunga mashairi ya arudhi kwa kuzingatia vipengele vya utunzi wa mashairi.	Anatunga kwa ubunifu mashairi ya arudhi ya kiwango cha juu kwa kuzingatia vipengele vya utunzi wa mashairi.	Anatunga mashairi ya arudhi kwa kuzingatia vipengele vya utunzi wa mashairi.	Anatunga mashairi ya arudhi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya utunzi wa mashairi.	Anatunga mashairi ya arudhi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya utunzi wa mashairi kwa kuongozwa.

FASIIH BUNILIZI NA KAZI ZA KIHALISIA

Viwango Vigezo	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Kuweza kuchambua bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vya uchambuzi.	Anachambua kwa utondoti bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vya uchambuzi.	Anachambua bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vya uchambuzi.	Anachambua kwa kiasi bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vya uchambuzi.	Anachambua kwa kiasi bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vya uchambuzi, kwa kuelekezwa.
Kuweza kuandika bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vifaavyo.	Anaandika kwa ubunifu bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vifaavyo.	Anaandika bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia vipengele vifaavyo.	Anaandika bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo.	Anaandika baadhi ya bunilizi na kazi za kihalisia kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo.

MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI

Mada	Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini	Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji	Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji
FASIHI SIMULIZI	• Uwasilishaji kwa mdomo • Mijadala • Uigizaji • Maswali na majibu • Majadiliano • Hotuba • Tathmini zilizoandikwa • Potifolio ya mwanafunzi • Shajara ya mwanafunzi • Mahojiano	• Kamusi • Majarida • Wageni waalikwa • Michoro na Picha • Video • Vitabu vya Fasihi simulizi • Chati • Kadi • Tovuti mbalimbali • Ramani za Google • Makavazi • Vibonzo • Vifaa vya kitamaduni k.v. vyombo vya muziki	• Tamasha za maigizo • Tamasha za muziki • Vibonzo • Tamasha za kitamaduni (k.v. harusi na posa) • Vilabu vya maigizo • Vilabu vya mijadala • Vilabu vya uandishi wa habari • Masimulizi ya hadithi

USHAIRI	• Kusoma kwa sauti • Kughani • Uigizaji • Maswali na majibu • Majadiliano • Kutoa hotuba • Tathmini zilizoandikwa	• Kamusi • Majarida • Wageni waalikwa • Michoro na Picha • Video • Diwani ya Mashairi • Majarida • Blogi	• Tamasha za maigizo • Tamasha za muziki • Vibonzo • Tamasha za kitamaduni (k.v. harusi na posa) • Vilabu vya maigizo • Vilabu vya mijadala • Vilabu vya uandishi wa habari • Ukariri wa mashairi
----------------	---	---	--

BUNILIZI NA KAZI ZA KIHALISIA	• Uwasilishaji kwa mdomo • Mijadala • Ugizaji • Maswali na majibu • Majadiliano • Hotuba • Tathmini zilizoandikwa • Potifolio ya mwanafunzi • Shajara ya mwanafunzi • Mahojiano • Utunzi wa tungo za fasihi	• Kamusi • Majarida • Wageni waalikwa • Michoro na Picha • Video • Riwaya • Hadithi fupi • Tamthilia • Wasifu • Majarida • Blogi • Vibonzo • Maleba	• Tamasha za maigizo • Tamasha za muziki • Vibonzo • Tamasha za kitamaduni (k.v. harusi na posa) • Vilabu vya maigizo • Vilabu vya mijadala • Vilabu vya uandishi wa habari
--------------------------------------	---	---	---